**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS; TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Unapojibu***:* ***SHULE YA SEKONDARI MACECHU,***
***Mkuu wa shule*** ***S.L.B 5668,***
***Mobile : 0654424272*** ***TANGA,***
***Tarehe ................................***
***Email***[macechuschool@gmail.com/ibrahimokash45@gmail.com](mailto:macechuschool@gmail.com) ***Tarehe ...................................***

**KUMB. NA. MAC/KID V/VOL I/ 01…………….**

Mwanafunzi…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………….

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO**
**MWAKA 2022/2023 TAHASUSI CBG/PCB**

1. Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kuingia Kidato cha…**TANO** katika shule hii.
2. Shule ipo ndani ya jiji la Tanga kata ya Chumbageni kilomita TATU kutoka stendi kuu ya mabasi-Tanga mjini. Hii ni shule ya bweni kwa wavulana wa kidato cha tano na sita tu.
3. Shule itafunguliwa tarehe **………………………..**.
4. **Usafiri: Ukishuka kituo cha mabasi kange panda Daladala za mjini, shuka stendi ya zamani kisha panda daladala za CHUMBAGENI-NGUVUMALI, Shuka kituo cha mabasi kisosora, uliza shule ilipo au panda Daladala za Amboni Mabokweni shuka kituo cha chumvini kisha uliza shule ilipo. Nauli ya daladala ni sh400 tu, Bodaboda sh1500 bajaji sh3000 au tax 5000 tu.**

***SHERIA ZA SHULE***

1. Heshima na adabu kwa viongozi, Wazazi, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
2. Utii kwa walimu, Wafanyakazi wasio walimu na viranja.
3. Kuwahi kufika shuleni na kutoondoka shuleni kabla ya shule kufungwa.
4. Kuzingatia ratiba ya shughuli za kila siku za Shule.
5. Kuwahi katika kila wito (utii kwa kengele)
6. Kuvaa sare ya shule madarasani, muda wa kazi na michezo.
7. Ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa
8. Hairuhusiwi kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe wala majumba ya wageni.
9. Ulevi wa aina yoyote ni marufuku.
10. Ugomvi na matusi ni mwiko
11. Wizi, kuharibu mali/kifaa cha shule au kuandika maandishi na michoro kwenye kuta za shule, milango n.k ni marufuku.
12. Kila mwanafunzi anatakiwa awe msafi.
13. Ni mwiko kutupa taka/karatasi au uchafu ovyo.

14. Urafiki wa kimapenzi hauruhusiwi.
15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuoa au kuolewa.
16. Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda nyumbani kwa wafanyakazi bila ruhusa
17. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia vyombo vya umeme Bwenini/darasani
18. Ni marufuku kwa mwanafunzi **kuwa na simu ya mkononi shuleni.**

***Ufafanuzi zaidi wa kina utatolewa mara ufikapo shuleni.***

**MIIKO MAALUMU: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE**

Mwanafunzi atakayepatikana na **makosa yafuatayo hatasamehewa, atafutwa shule mara moja**.

(a) Uasherati na Ushoga.
(b) Ubakaji.
(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji sigara/bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
(d) Kupigana au kupiga.
(e) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(f) Kudharau bendera ya Taifa.
(g) Kuoa au kuolewa.
(h) Kumpa mimba msichana ndani au nje ya shule.
(i) Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvunja amani na usalama wa shule au watu.
(j) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(k) Mwanafunzi kuwa na **simu ya mkononi**
(l) Kashfa ya aina yoyote kwa Taifa kama kudharau nembo ya Kitaifa (Sikukuu za Kitaifa, mikutano, wimbo wa Taifa, maandamano, n.k).
(m) Wizi (kuiba).
(n) Kuendesha magendo au ulanguzi wa aina yoyote.
(o) Kosa la jinai, kosa likidhibitishwa na polisi au mahakamani.
(p) Kulala nje ya shule bila ruhusa.
(q) Kutoa mimba au kushiriki katika zoezi la kutoa mimba.
(r) Mwanafunzi kubana suruali au shati (Modo)

**A. ULIPAJI WA KARO NA MICHANGO**

**(a) KARO YA SHULE**

Karo ya shule ni **Tsh. 70,000/= kwa mwaka au Tsh 35,000/= kwa nusu mwaka**; ilipwe kwenye tawi lolote la benki ya NMB.Kupitia account namba 41701200087

**MICHANGO MINGINE.**

| ***Na.*** | ***MICHANGO*** | ***KIASI CHA FEDHA (Tshs.)*** |
|---|---|---|
| 1. | Tahadhari | 10,000/= |
| 2 | Kitambulisho | 3,000/= |
| 3. | Matibabu | 15,000/= |
| 4. | Ulinzi | 15,000/= |
| 5. | Taaluma | 20,000/= |
| 6. | Upishi | 15,000/= |
| 7. | Ukarabati | 30,000/= |
| 9 | Samani | 10,000/= |
| | **JUMLA** | 118,000/= |

**JUMLA YA MALIPO YOTE.**

**Jumla ya malipo yote ni Tsh 188,000/= kwa mwanafunzi aliyelipa ada Tsh 70,000/= au 153,000/= kwa mwanafunzi aliyelipa ada Tsh 35,000/=**

Fedha zote ziwekwe katika tawi lolote la benki ya NMB Akaunti namba 41701200087 Jina la Akaunti ***HEADMASTER MACECHU SECONDARY SCHOOL FUND***.

**MWANAFUNZI ANATAKIWA AKABIDHI BANK-PAY-IN SLIP YA MALIPO SIKU YA KURIPOTI SHULE**

**MAHITAJI YA NYONGEZA YA MWANAFUNZI**

Mahitaji yafuatayo ni kwa ajili ya vifaa na matumizi ya mwanafunzi. Fedha hizi zitalipwa shuleni na siyo Bank.

| **Na.** | *MICHANGO* | *KIASI CHA FEDHA (Tshs.)* |
|---|---|---|
| 1. | T-shirt ya shule | 12,000/= |
| 2. | Suruali 2 @17,000/= | 34,000/= |
| 3. | Shuka 2 @ 7,500/= | 15,000/= |
| 4. | Sweta | 15,000/= |
| | **JUMLA Tshs.** | **76,000/=** |

**SARE YA SHULE (Mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo siku ya kuripoti shule)**

i. Mashati mawili meupe (tetron) ya mikono mifupi mfuko mmoja.
ii. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba jozi mbili visiwe na visigino virefu.Safari boots na viatu vya wazi haviruhusiwi.
iii. Soksi jozi mbili au zaidi ziwe za rangi nyeupe.
iv. Mkanda wa ngozi mweusi wenye upana wa kawaida usiwe na charter yeyote.
v. Atakaye kuja na nguo isiyo sare ya shule au isiyo rasmi atarudishwa nyumbani.
vi. Mwanafunzi aje na suruali ya rangi ya nyeusi na tisheti ya rangi nyeupe.
(mwanafunzi aje na mavazi hayo anaporipoti shuleni)
Suruali iwe saizi ya kawaida isiyoshika mwili (kimodo) inchi 17 upana usawa wa kuanzia soli ya kiatu, yenye mkunjo kwa chini (turn up) na isiwe na urembo wowote
(Mlegezo hautakiwi)
vii. Mwanafunzi atokapo nje ya shule anatakiwa kuvaa sare ya shule.
viii. Nguo za michezo; mwanafunzi aje na:
(a) Track suit ya blue au bukta ya blue au fulana ya bluu (Jezi)
(b) Raba jozi moja

***MAELEZO YA LIKIZO***

- Wakati wa likizo za mwisho wa Mhula, **NI LAZIMA** mwanafunzi aondoke/arudi nyumbani, hivyo basi, hakikisha unampatia/umemtumia mwanao nauli ya kurudi nyumbani; shule haiwajibiki kumpatia mwanafunzi nauli/chakula na malazi wakati wa likizo.

***USAFI BINAFSI WA MWILI***

- Nywele fupi za kuchana kwa kitana kidogo.
- Ndevu na mustachi havitakiwi.
- Kuoga kila siku ni lazima.
- Huruhusiwi kufuga kucha.
- Kuvaa kofia, bangili, hereni, kipini, kidani (Mkufu) na kikuku haviruhusiwi shuleni.

***UNUNUE VIFAA VIFUATAVYO NA UJE NAVYO SIKU YA KURIPOTI SHULE***

- Mopa Moja, soft broom moja na fagio la chelewa moja
- Ndoo moja ndogo ya plastiki kwa ajili ya usafi.
- Madaftari nane (8) counter book three quires) na kalamu nyeusi. au blue za kutosha.
- Mathematical set
- Sanduku la bati, masanduku na mabegi mengine hayaruhusiwi.
- Karatasi rimu (2) mbili.(Photocopy Paper)
- Scientific calculator moja (1)
- Picha nne za mwanafunzi PASSPORT SIZE
- Aje na tochi inayotumia betrii
- Dissecting kit

***VIFAA VYA MALAZI NA CHAKULA***

- Godoro jipya la sponji lenye upana wa futi mbili na nusu 2 ½ unene wa nchi 3 na urefu wa futi sita (6)
- Mto
- Sahani, kikombe, kijiko na bakuli
- Chandarua cha rangi blue
- Begi la darasani la kubebea madaftari.

***ANGALIZO:***
Mwanafunzi aje na mahitaji yote kama ilivyoorodheshwa hapo juu vinginevyo hatapokelewa.

***VIFAA NA MAHITAJI MENGINE***

- Fedha za mfukoni (pocket money)
- Ni muhimu kuwa na fedha za mfukoni ili uweze kujinunulia vifaa muhimu. Fedha hizo mwanafunzi atahifadhi mwenyewe mwanafunzi anashauriwa kufungua akaunti benki. Na shule itamsaidia katika hili mara tu atakapofika shuleni.
- Mzazi mpatie mwanao elfu kumi (10,000) kwaajili ya kufungua akaunti hakuna mwanafunzi anaeruhusiwa kukaa na pesa zaidi ya elfu tatu (3000) bwenini. **FEDHA ZOTE AHIFADHI BENKI**

***MAMBO MENGINE MUHIMU***

- Unapaswa kuja na fomu zilizoambatanishwa na barua hii zikiwa zimejazwa
- Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii utakabidhi kwa Mkuu wa shule mara utakapo ripoti shule.
- Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria za shule, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa
- Aje na nakala ya result slip.

**HITIMISHO**

Tafadhali soma kwa makini maelekezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Mwanafunzi aripoti shuleni kabla ya saa 12 Jioni.

KARIBU SANA

………………………

MKUU WA SHULE

Nakala:-

1. Katibu Mkuu
   Wizara Ya Elimu na mafunzo ya Ufundi
   S.L.B 9121, DAR ES SALAAM

2. Mkaguzi Mkuu wa Shule,
   Kanda ya Kaskazini Mashariki,
   S.L.P. 460,
   **MOSHI**

3. Afisa Elimu (M) ,
   Mkoa wa Tanga
   S.L.P. 313, TANGA

4. AfisaElimu Sekondari (W),
   Jiji la Tanga
   S.L.P. 178-TANGA

## ***HISTORIA FUPI YA MWANAFUNZI (PERSONAL PARTICULARS)***

***SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI***

| |
|---|
| **PICHA YA MWANAFUNZI** |

1. Jina kamili la mwanafunzi ____________________________________________
   (a) Tarehe ya kuzaliwa ____________________________________________
   (b) Kijiji / mtaa alichozaliwa/Mji ________________wilaya ________________
   Dini /dhehebu____________________________________________________
   URAIA ____________________________________________________________

2. (a) Shule ya sekondari uliyotoka ___________________________________________
   Anuani ya shule ya sekondari uliyotoka ________________________________

| |
|---|
| **PICHA YA MZAZI/MLEZI** |

3. (b) Jina kamili baba /Mlezi ……………………………UHUSIANO________________
   (c) Hai/Amefariki ____________________________________________________
   (d) Anuani ya Mzazi/Mlezi ____________________________________________
   (e) Mahali anapoishi …………………………………mtaa wa____________________
   Kazi anayofanya ____________________________________________________
   (f) Jina la atakayekulipia karo__________________________________________
   Anuani yake________________________________________________________
4. **AFYA:** (i) Taja magonjwa yote makubwa yaliyowahi kukushika (k.m kifafa, pumu, kifua kikuu )

_______________________________________________________________________

(ii) Una upungufu au matatizo yoyote ya viungo (mfano macho, kilema n.k.) _____
_______________________________________________________________________

***SEHEMU YA PILI: UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI***

Ninathibitisha kwamba maelezo aliyoyatoa mwanafunzi katika karatasi yote ni sahihi.
***Jina la Mzazi/Mlezi*** ______________________________________________________

***NAMBA YA SIMU YA MKONONI***_____________________________________________________

SAHIHI____________________________________TAREHE_______________________________

***SEHEMU YA TATU : UTHIBITISHO WA AFISA MTENDAJI KATA***

**Ninathibitisha kuwa mwanafunzi mtajwa hapo juu ni raia Wa Tanzania na anaishi ndani ya kata hii.**

Jina la Afisa Mtendaji_________________ KATA YA________________________________

SAHIHI_______________________________TAREHE__________________________

Tarehe ………………………………

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATIONS AND LOCAL GOVERMENTS**

# ***REQUEST OF MEDICAL EXAMINATION***

**MACECHU SEC. SCHOOL,**
**P.O.BOX 5668,**
**TANGA**

TO: Medical Officer
……………………………………………..
……………………………………………..

**RE : THE STUDENT**______________________________________________________________

Please examine the above named as to his fitness- mentally and physical for full time secondary education.
In boarding school.

**MEDICAL CERTIFICATE**
**(To be completed by a Government Officer).**

I Have examined the above named for secondary education; with the following findings:
A: Eye sight:………………………………………………………….(B) Hearing………………………………………………………….
C: Limbs:…………………………………………………………………..(D)Venereal Diseases:……………………………………..
E: Seech:…………………………………………………………………(F)Leprosy…………………………………………………
G: Epillepsy…………………………………………………………….(H)STDS:……………………………………………………..……..
(ii) Neuroses:……………………………………………………….(iii)Other serious diseases:……………………………….
ANY ADDITIONAL INFORMATION eg. Physical defects, infections disease (eg. HIV/ADS &STDS Impair ment treatment/ongoing treatment/undergo accident……………………………………………………………………..
Station: ____________________ ____ NAME OF MEDICAL OFFICER ________________________

___________Designation:_________________________________Stamp____________________

DATE___________________________________________________________________________

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS MKUU**
**TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI MACECHU**
**S.L.P. 5668,**
**TANGA**

# FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA MWONGOZO WA SHULE

Mimi ………………………………………………………………………………………………………… nakubali kupokea nafasi ya kidato cha V niliyopewa katika shule ya sekondari MACECHU. Naahidi kuwa nitatii sheria/mwongozo wa shule, nitakuwa mkunjufu vile ipasavyo. Nitafika shuleni saa 12:00 asubuhi bila kuchelewa. Nitafuata ratiba na kuwepo katika eneo kama ratiba inavyoelekeza. Sitatoroka ovyo, wala kupiga kelele na Nitafuata taratibu za shule nitakavyoelekezwa na walimu au Uongozi wa shule.

**SAINI YA MWANAFUNZI ____________________TAREHE______________________________________**
**ANUANI YA KUDUMU ……………………………………………………………………………………………………………..**
**…………………………………………………………………………………………………………………………………………**

## SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi ………………………………………………………………………………………………………… Mzazi/Mlezi ninakubali kumpatia mwanangu mahitaji yote vitu vinavyotakiwa kuja navyo shuleni. Nitashirikiana na walimu kikamilifu katika kumwongoza, kumlea kumuwezesha na kumpa nafasi ya kusoma hata awapo nyumbani.

***NITAFUATILIA MAENDELEO YAKE KWA KARIBU NA KUCHUKUA HATUA MATHUBUTI KILA AFANYAPO UZEMBE.***

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI** ……………………………………TAREHE______________________________________

**ANUANI YA KUDUMU**

________________________________________________________________________
………………………………………………………………………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………………………………………………………………

**MAONI YA MKUU WA SHULE**

………………………………………………………………………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………………………………